PDF Compressor Free Version

102/1 MK
KISWAHILI
KARATASI YA 1
INSHA
MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA
MACHI 2021

**THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL**

**KENYA CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION**

**KISWAHILI**

KARATASI YA 1

# Mwongozo wa Kusahihishia

**(SIRI)**

**MWONGOZO HUU WA KUSAHIHISHIA NI MILKI YA BARAZA LA MITIHANI YA KITAIFA LA KENYA (KNEC) NA SHARTI KUREJESHWA KWA BARAZA HILI BAADA YA USAHIHISHAJI**

**Mwongozo huu wa kusahihishia una kurasa 4 zilizopigwa chapa.**

©2021 The Kenya National Examinations Council

1. Hii ni ripoti.

Yafuatayo yazingatiwe:

**(a) Muundo**

PDF Compressor Free Version

Sura ya ripoti idhihirike.

(i) Kichwa – kionyeshe kiini cha uchunguzi.

(ii) Utangulizi

- Mtahiniwa ataje jopokazi: wanachama walioteuliwa, aliyeteua jopokazi
- Hadidu za rejea (Masharti na mipaka ya utekelezaji wa kazi iliyopangiwa jopokazi.)
- Sampuli lengwa - habari zilikokusanywa.
- Njia za ukusanyaji – hojaji, mahojiano, majadiliano kwenye vikundi.

(iii) Mwili – hoja zijadiliwe humu; vichwa vidogo vitumiwe.

a) Sababu/mapuuza/Matokeo

~~(iv) Hitimisho~~ Hoja

~~(v)~~ b) Mapendekezo

c) Hitimisho

(vi) d) Sahihi, jina, tarehe (Kimalizio)

**(b) Maudhui**

Baadhi ya hoja ni:

(i) Msisitizo mkubwa kwenye masomo ya kiakademia.

(ii) Kutokuwa na vielelezo tosha vya watu waliofanikiwa kwa kufuatia masomo ya aina hii.

(iii) Masomo haya kutohimizwa katika shule nyingi kwa sababu ya ukosefu wa vifaa.

(iv) Ukosefu wa walimu waliohitimu katika taaluma hizi.

(v) Shinikizo kutoka kwa wazazi – wanafunzi wajishughulishe na masomo mengine.

(vi) Mtazamo hasi kuwa baadhi ya masomo kama vile ufundi wa mabomba ni duni.

(vii) Hapajawa na mfumo bayana unaoonyesha hatua ambazo mwanafunzi/mwanagenzi atapitia hadi pengine Chuo Kikuu.

(viii) Mafunzo mengine ya kiufundi ni ghali.

(ix) Vyuo vichache vya kiufundi katika sehemu za mashambani.

(x) Vyuo vingine vya kiufundi vimegeuzwa kuwa vyuo vikuu, hivyo wanafunzi kutoona umuhimu wa vyuo vya kiufundi.

(xi) Baadhi huenda wasimudu masomo ya kisayansi, hivyo kukata tamaa.

xii) Masomo haya yanahitaji mtaji ndipo anayesomea apate ajira

xiii) Mtazamo potovu kuwa masomo haya ni ya mapato ya chini.

xiv) Walimu kuwavunja wanafunzi moyo.

xv) Masomo haya hayana mvuto kwa wanafunzi.

xvi) Masomo haya huwafunga wanafunzi kuhusika wenyewe

xvii) Mtazamo hasi wa kijinsia, kitamaduni, kiitikadi n.k.

N/B Hoja zingine ziko wazi.

* Apewe mkwaju wa hoja

PDF Compressor Free Version

Mtahiniwa atoe angaa mapendekezo mawili. Kwa mfano:

(i) Mtaala usisitize masomo ya kiufundi kuanzia ngazi za chini.

(ii) Vyuo vya Ualimu vihusishe ufundishaji wa masomo ya kiufundi.

(iii) Serikali iongeze ufadhili kwa masomo ya kiufundi.

(iv) Kuwe na mfumo bayana unaoonyesha taaluma ambayo mwanafunzi atasomea akifuatia masomo ya kiufundi.

2. Makala yaonyeshe umuhimu wa magazeti.
Sura ya Makala idhihirike.
Baadhi ya hoja ni:

(i) Kujuza kuhusu yanayojiri nchini/ulimwenguni.
(ii) Kupalilia usomaji wa mapana.
(iii) Hukuza ubunifu – mwanafunzi atajifunza mitindo mbalimbali ya uandishi.
(iv) Kufunzia/kujifunzia sajili ya magazeti.
(v) Baadhi huwa na safu ya kufunzia vipengele vya lugha.
(vi) Hukuza stadi za kuhariri.
(vii) Hupalilia uwazaji wa kina, kwa mfano kupitia kujaza mraba.
(viii) Kupalilia mazoea ya kusoma.
(ix) Kufanikisha somo la maktaba.
(x) Kupalilia mbinu za kitafiti/mazoea ya kudadisi.

3. Hii ni insha ya Methali.
Kisa kidhihirishe maana ifuatayo:
Mtu asipotia bidii katika jambo matokeo yake huwa hafifu.

**AU**

Kiasi cha kufanikiwa katika jambo hutegemea matayarisho/mikakati ambayo inawekwa.

Baadhi ya hali ambazo zinaweza kujitokeza ni:

(i) Mwanafunzi kutojitayarisha ipasavyo kwa ajili ya mtihani na hatimaye kupata alama zisizoridhisha.

(ii) Wakulima wakose kujiandaa ipasavyo, mwishowe wapate mavuno haba.

(iii) Shirika likose kuweka mikakati ifaayo kuimarisha pato lake; lisipate faida, mwishowe lifilisike.

(iv) Mlezi kutowaelekeza watoto ipasavyo, watoto kuinukia kuwa wasiotegemewa.

(v) Mwajiri kutojaribu kuimarisha uhusiano wake na waajiriwa wake, migogoro izidi, uzalishaji mali uathirike vibaya.

PDF Compressor Free Version

**Tanbihi**

1. Vipengele vitatu vya kimuundo vijitokeze; Utangulizi, mwili, hitimisho.
2. Kichwa cha makala kidhihirike.
3. Sharti insha idhihirishe juhudi hafifu/mikakati hafifu/ukosefu wa kujiandaa, na baadaye hali/matokeo yasiyoridhisha.

4. Atakayejihusisha au atakayehusisha mtu mwingine atakuwa amejibu swali
5. Ashughulikie pande zote mbili za methali. Atakayeshughulikia upande mmoja
4. asipite alama 10(C).

Hii ni insha ya kibunilizi.

Mtahiniwa atunge kisa ambacho kinaoana na mwanzo huu.

Usimulizi unaweza kubainisha hali zifuatazo:

(i) Msimulizi asimulie yaliyotokea baada ya kuwasili, labda hata anaibiwa.

(ii) Msimulizi aonyeshe alikoenda baada ya kuwasili, labda anapokelewa na mwenyeji wake; kisha asimulie maisha yake huko kwa mwenyeji wake.

(iii) Anaweza kuwa anapitia hapa tu; pengine anatoka garini kupumzika kabla ya kuendelea na safari yake. Baadaye anaendeleza usimulizi wake hadi panapoishia safari.

(iv) Msimulizi anaweza kuanza kwa kauli hizi, kisha akaturudisha nyuma kusimulia kisa ambacho kinamleta hapa. (mbinu rejeshi)

(v) Anaweza pia kusimulia maisha ya watu wa mji huu.

vi) Akikosa kunakili dondoo, lakini amelenga kisa, aadhibiwe kimtindo.

vii) Akiandika kisa ndotoni, atakuwa amejibu swali, bora ioane na mahitaji ya swali.

viii) Si lazima ataje mji wa Taparuku.

ix) Kisa kiwe na kichwa.